# Kristo 2



# KRISTO 2



**MWANDISHI:**
Ben Avery

**PENSELI:**
Sergio Cariello

**INKS:**
Sergio Cariello

**BARUA:**
Tabitha Rani

**RANGI:**
Fabricio Guerra

**MTAFSIRI:**
Marci Onsinyo

**MHARIRI:**
Reuben Onsinyo

**KUBUNI:**
Lisa McMahon

**MCHAPISHAJI:**
Kingstone Comics

---

Kimechapishwa na Comic Bible Society
Hakimiliki @2021

COMIC BIBLE SOCIETY

Kingstone Comics inahifadhi hakimiliki ya kitabu hiki ilivyoruhusiwa na sheria ya hakimiliki za Marekani.

Nakala za kuchapichwa na za dijitali za toleo hili la Kiswahili zaweza kusambazwa bure bila adhabu chini ya leseni ya Creative Commons.


MWEZI MMOJA BAADA YA KUZALIWA KWA YESU, MARIA NA YOSEFU WALISAFIRI KUTOKA BETLEHEMU HADI YERUSALEMU KUMTAMBULISHA MTOTO NA KUTOA KAFARA WALIVYOTARAJIWA.
TUNGEPENDA NJIWA WAWILI TAFADHALI.
AH, NDIO!
MUMEKUJA KUMTOLEA MVULANA WENU KAFARA, SIO?
NDIO.
TUTACHUKUA HAWA WAWILI.
KAFARA NDOGO AJABU...
HATUWEZI KUMUDU MWANA KONDOO, MARIA.
NAJUA. NAJUA.
BINAMU YANGU ANAFKIRIA NAWEZA KUPATA KAZI ZA USEREMALA HUKO BETLEHEMU.
UISHI BETLEHEMU?
SIJUI...
HATUTAKAA KWA MDA MREFU LAKINI NTAWEZA KUTENGENEZA HELA ZA KUTOSHA KUWAANGALIA WEWE NA MTOTO, LABDA TUPATE NYUMBA...
TUNA NYUMBA! ULIIJENGA WEWE!

LUKA 2:22-24


NAJUA.
LAKINI KAMA KUNA KAZI NAWEZA KUFANYA BETLEHEMU ANGALAU TUIFKIRIE.
NATAKA KILICHO BORA KWA JAMII YETU.
NTALIWAZA.
TAZAMA VIZURI YESU.
UTAKUWA UKIPAONA MAHALI HAPA SANA.
FAMILIA ZETU HUJA HAPA KILA MWAKA KWA SHEREHE YA PASAKA.
SAMAHANI!
MWANAO!
NIMEMUONA MWANAO!
KUNA JAMBO NAWEZA KUKUSAIDIA NALO?
YAWEZA KUWA VIGUMU KWAKO KUAMINI, LAKINI NILIAMBIWA NIJE HAPA KUMTAFUTA MWANAO!
WAZUNGUMZIA NINI?
POLE. JINA LANGU NI SIMIONI. BWANA ALINIAMBIA NIJE HAPA.
SIKUJUA KWA NINI LAKINI KWA KUWA NIMEMUONA MWANAO-- YEYE NDIYE SABABU!
POLE! ACHA NIELEZE.
HAPO KALE, MUNGU ALIONGEA NAMI. ALINIAMBIA SINGEKATA ROHO MPAKA NIMUONE ATAKAYEKUWA FARAJA NA ATAKAYELIWAZA ISRAELI!
MWANAO! YEYE NDIYE!
NAWEZA KUMBEBA?
NDIO. BILA SHAKA.



LUKA 2:23-27



JINA LAKE...
JINA LAKE NANI?
JINA LAKE NI YESU.
YESU...SIAMINI SIKU HII HATIMAYE IMEFIKA!
MARIA?
NI SAWA YOSEFU.
NI SAWA.
MUNGU! MUNGU MKUU, NI VILE VILE ULIVYOAHIDI!
NAWEZA KUFA KWA AMANI SASA NIKIJUA UMETUMA MASIHI WAKO!
MACHO YANGU YANATAUTAZAMA UKOMBOZI WAKO!
MACHO YANGU YANAMUONA ATAKAYEKUWA TAA KWA WAYUNANI!
MACHO YANGU YAMUONA ATAKAYENGAA MWANGAZA WA UTUKUFU WAKO KWA WATU WAKO WAISRAELI!


LUKA 2:28-32


MTOTO HUYU ATAKUA MKUU SIKU ZIJAZO.
ATASABABISHA KUINUKA NA KUANGUKA KWA WATU WENGI ISRAELI.
MATAMSHI YAKE YATAINGIA KWENYE MIOYO NA ROHO ZA WOTE WAMSKIAO, KUTHIHIRISHA MAWAZO YAO YA KWELI NA MIOYO YAO.
KISHA...
NA SIME ITAIDUNGA ROHO YAKO PIA.


ANNA! NJOO UPESI!
ANNA NI NABII! ANAFAA AMUONE MTOTO HUYU PIA!
MTOTO HUYU, SIMIONI!
UNAJUA MTOTO HUYU NI NANI, SIO?
NI ULICHOKUA UKIKINGOJEA!
NI ALICHOAHIDI BWANA UTAKIONA!
MACHO YANGU MAKUU!
LEO NI LEO!
MASIHI WA BWANA! MKOMBOZI WA BWANA!
WOTE WAUTAFUTAO UKOMBOZI WA YERUSALEMU MSIZIDI KUTAFUTA ZAIDI YA HAPA!
YUKO HAPA! HUYU KIJANA MDOGO!
YOSEFU TWENDE NDANI...
TULIFANYE LILILOTULETA.
KWA HIYO MARIA NA YOSEFU WALITOA KAFARA ZAO, KAFARA MOJA YA UTAKASAJI NA MOJA YA KUWEKA WAKFU, INAVYOPASWA KATIKA VITABU VYA SHERIA.


MIAKA MIWILI BAADAYE.
SAA ZENGINE NAJIULIZA KAMA INGALIKUA TOFAUTI KAMA TUNGERUDI NAZARETI.
MIMI PIA MARIA LAKINI INAONEKANA TUTAFANIKIWA.
NAZARETI HAKUNGEKUA NA VIBARUA VINGI MAANAKE INGEBIDI NIGAWANE NA BABANGU NA KAKA ZANGU.
HAPA KWA SASA NAPATA MAPATO MAZURI YETU SISI.
NDIO LAKINI SISI WATATU TWABABANYA TU!
JE TUKIPATA WATOTO WENGINE?
LABDA WAJUA VYENGINE, ILA KWA SASA TUKO WATATU TU.
SISEMI KUWA SITAKI KWENDA NYUMBANI.
NI KWAMBA BADO SITAKI KUONDOKA BETLEHEMU.
YOSEFU, NAWAKOSA FAMILIA YANGU. NA NINATAKA KUISHI KWENYE NYUMBA ULIYOTUJENGEA!
KUGAWANA VIBARUA NA JAMII YAKO SIO VIBAYA, IWAPO HAPO NDIPO MOJAWAPO PA MAHALI WATU NAZARETI WANAWEZA KUPATA USEREMALA.
NA NINGEJIHISI SALAMA KUISHI KARIBU NA JAMII ZETU--
HUO NI MLIO WA NINI?
FARASI. WENGI. KAMA AMBAYE MSAFARA.
YESU YUKO HUKO NJE...
YESU!
YESU!




MTOTO HUYU.
TULIONA NYOTA ILIYOTUONGOZA HAPA.
TULIFAHAMU MTOTO WA UMUHIMU MKUU KAZALIWA.
NA HUYU NI MTOTO HUYO, SIO?
JINA LAKE NI YESU.
TUMEKIPATA TUNACHOKITAFUTA!
ASIFIWE MTOTO WA KIFALME!
ASIFIWE MASIHI!
*ASIFIWE MASIHI!*



MATHAYO 2:11


SAMHANI KWA NYUMBA YETU DUNI TAFADHALI.
DUNI? HATA! NYUMBA YOYOTE IMKINGAYO MFALME WA KIMUNGU SIO DUNI!
TWAJUA MTOTO WAKO NI NANI.
TWAELEWA AMAANISHA NINI.
TULIPOONA NYOTA TULIJIULIZA KILE ILICHOMAANISHA NA TUKATAFUTA UNABII KWENYE REKODI ZETU UTAKAOTUONGOZA KWA JIBU!
"JIBU LILIPATIKANA KWA MAANDIKO FLANI YALIYOKUWA YAMEWEKWA KWENYE MAKTABA YETU KWA MAMIA YA MIAKA NA MMOJA WA WATU WENU."
"TULIIFUATA NYOTA NA TULIVYOTARAJIA ILITUONGOZA HADI KWA NCHI YENU!"
"LAKINI ILIPOTUPOTELEA TULIENDA YERUSALEMU TULIPODHANIA KAWAIDA MTOTO WA KIFALME ANGALIKUWA!"
"MFALME WENU ALITUSAIDIA KIDOGO LAKINI WASHAURI WAKE WALIPATA UNABII MWENGINE ULIOASHIRIA BETLEHEMU."
"MFALME HERODE ALITUTUMA TWENDE AKISEMA,"
TAFADHALI ENDENI! MTAFUTE MWANA HUYU NA MUMBARIKI NA KUMWABUDU! LAKINI MSISAHAU KURUDI HAPA KUNIAMBIA ALIKO ILI MIMI PIA NIENDE NIKAMWABUDU!
"HAPO NYOTA ILIKUA IMEREGEA KWA HIYO TUNGEIFUATA TENA NA KWELI ILITUONGOZA HAPA."
"KUWAPATA HAIKUWA SHIDA. YAONEKANA ALIPOZALIWA KULIKUA NA MFURUKUTANO KATIKA KIJIJI HICHI KIIDOGO!"
"KATI YA NYOTA NA WAKAAZI NA HADITHI ZAO ZA MALAIKA NA MANABII WENU, TULIJUA HATUMTAFUTI TU MTOTO WA KIFALME ILA KITU KIKUU NA NADRA ZAIDI."






MATHAYO 2:11-12


WAKO WAPI!
*WAKO WAPI!!!*
BWANA, WALIONDOKA KWENDA BETLEHEMU PINDI TU WALIPOFIKA.
KUTOKANA NA HABARI TULIOIPATA WALIONDOKA MDA MREFU ULIOPITA KIASI CHA KWAMBA WALIPASWA KUWA WASHAFIKA HAPA ILHALI--
ILHALI, HAWAKO HAPA BADO!!!
HAWAKO HAPA!!!
*HAWAKO HAPA!!!*
IKIJULIKANA KUWA HAWA WATAA-- HAWA "WAKUZA MFALME" --WAMETII MTOTO--






MATHAYO 2:16-18


BETLEHEMU.
YOSEFU AMKA!
HARAKISHA UWAONDOE MKEO NA MWANAO KUTOKA MAHALI HAPA.
LAZIMA MUENDE MISRI MKAE HUKO MPAKA NITAPOWAAMBIA MRUDI.
NINI?
MFALME HERODE ATAKA KUMUUA MTOTO. LAZIMA MUENDE.
LAKINI...
ITAKUA VIP...
MARIA?
KUNA NINI YOSEFU?
AMKA UPESI.
MALAIKA AMENIAMBIA MFALME HERODE ATAKA KUMUUA YESU.
LAZIMA TUONDOKE HAPA. SASA HIVI.


KWA HIYO MARIA, YOSEFU NA YESU WAKAFUATA MAAGIZO YA MALAIKA...
TAFADHALI BWANA TWAHITAJI MAHALI PA KUKAA LEO USIKU.
NINA CHUMBA LAKINI KUKUTAYARISHIA MASAA HAYA...
TUTAKUPA SHILINGI HII YA DHAHABU.
HIYO ITAKUWA MURWA!
...PIA WANAJESHI WA HERODE WALIVYOFUATA MAAGIZO.
HUKO MISRI WALIJIJENGEA MAISHA WAKITUMIA UJUZI WA YOSEFU WA USEREMALA NA HELA KUTOKA KWA ZAWADI ZA WATAALAMU.


NGOME YA MFALME HERODE.
MDA MFUPI BAADAYE.
...KWA HIYO, MKUBWA KAISARI, NINA--AA--PENDEKEZA UGAWE NCHI YA WAYAHUDI NILIVYOELEZA.
"...NILIVYOELEZA."
BABA!
HUU NI USALITI WA AINA GANI?
UNAPANGA KUNIFANYA NIGAWE NCHI YENU NA PHILIP NA ARCHELAUS?
KIJANA!
NINA--AAH--NINAJUA KILICHO BORA! KWAKO WEWE NA NCHI YANGU!
BABA UNANIJUA NINAVYOJIJUA, HII SIO KUHUSU LILILO BORA KWANGU AU NCHI HII.
AH. HARUFU HIO NI YA NINI? CHUMBA HIKI KIZIMA CHANUKA UVUNDO!
ONA, EWE MFALME MKUU HERODE, MFALME WA WAYAHUDI!
BABA ULISHINDA KILA KUKICHA UKILINDA MAHALA PAKO KWENYE UFALME HUU!
UMEWAUA WAKE NA WATOTO NA HATA WANAO KATIKA MINAJILI YA KUSHIKILIA NAFASI YAKO KAMA MFALME!
LAKINI JIANGALIE BABA, UMEFELI!
UNANYANG'ANYWA UFALME VILE VILE!
WE RUDI HAPA!
NIANDAME KAMA MUME!
WE MJINGA, MJINGA... AAAHH






MATHAYO 2:19-21


YESU ALIPOKUWA MIAKA KUMI NA MIWILI WAZAZI WAKE, KAMA ILIVYOKUWA DESTURI YAO, WALISAFIRI KWENDA YERUSALEMU KWA SHEREHE YA PASAKA NA FAMILIA YAO.
KURUDI NYUMBANI NAZARETI BAADA YA PASAKA MARIA NA YOSEFU WALIACHANA ILIVYOKUWA DESTURI, WAUME WALISAFIRI NYUMA MWA KIKUNDI NA WAKE NA WATOTO MBELE.
UKO SAWA?
MARIA, NIMEKAA KWENYE PUNDA HUYU KARIBIA SIKU NZIMA!
WE NIAMBIE!
ACHA NIKUSAIDIE. WAEZA KUNYOSHA MISULI.
NAJUA ILIVYO. NISHASAFIRI HIVI MBELENI PIA.
WEWE? MIFUPA YAKO IKIZEEKA KAMA HII YANGU UTAELEWA.
NILIKUA NA MIMBA YA YESU WAKATI HUO
UNGEDHANI BAADA YA KILICHOMKUMBA ZAKARIA NINGEKAA KIMYA!
ASANTE KWA KUTEMBEA NAMI.
HUU NI MWAKA WA KWANZA YOHANA WANGU ANGETEMBEA NA WAUME NA HAKUIWACHA FURSA HIYO.
NI SAFARI YA UPWEKE BAADA YA KUWA NAYE MIAKA KUMI NA MIWILI ILIYOPITA.


WAFKIRIA ATAZIFUATA NYAYO ZA BABAKE KAMA KUHANI?
ATAFUATA NYAYO ZA BABAKE?
NDIO
KAMA KUHANI?
HAPANA.
ANAFANYA VIZURI MASOMONI KULIKO WENGI WA WAVULANA WENZAKE.
LAKINI...HAFAI.
YUKO...HURU SANA.
WEWE TU WAEZA KUELEWA.
HATIMA YAKE NI YA KITU TOFAUTI.
KWA HIYO NDIO, ATAKUWA KAMA BABAKE AKIONGOZA WATU KWA BWANA WETU.
LAKINI HAITAKUWA KUTOKA NDANI YA HEKALU.
NAJUA UNACHOMAANISHA.
NA NAOGOPA UNACHOMAANISHA.
MALAIKA WALILETA UJUMBE WA KUZALIWA KWA MWANANGU NA KUTUTAHADHARISHA KUTOKA BETLEHEMU KWA SABABU HERODE ALITAKA KUMUUA MWANANGU!
NABII YERUSALEMU ALITABIRI KUHUSU VITENDO VYA AJABU YESU ANGETENDA KISHA AKATABIRI YA KUWA UPANGA UNGENICHOMA ROHO!
STAKI KUMPOTEZA MWANANGU!
MARIA, MARIA...


YESU NA YOHANA PIA NADHANIA WOTE WAWILI NI ZAIDI YA WANA WETU TU!
--NA WATAMAANISHA ZAIDI KWA WATU WENGI ZAIDI!
LABDA LAKINI YEYE NI MWANANGU NA MIMI NI MAMAKE--
MAMA?
KUNA NINI MPENDWA?
UMEMUONA YESU?
ALICHEZA NAMI TULIPOSAFIRI KWENDA YERUSALEMU NA NILITUMAINI ATACHEZA NAMI KURUDI NYUMBANI PIA!
LAKINI SIJUI ALIPO!
NA NINAKUAPIA NG'OMBE ALIKUA MATOPENI MPAKA TUMBONI LAKINI PINDI TU HARUN ALIPOKANYAGA TOPENI KUWEKA KAMBA KWENYE SHINGO YA JITU LILE ILI WAMVUTE NJE…
...ALIZAMA MPAKA SHINGONI!
YOSEFU!
HAYA, YOSEFU!
MKEO AKUITA!
NA SINA BUDI KUJIBU! YAONESHA ANA WASIWASI


MARIA, KUNA NINI?
YESU YUKO WAPI? YUKO NAWE?
NINI? HAPANA, YUKO NAWE!
HAYUKO NA WAKE NA WATOTO NA VILE AMEHITIMU KIUMRI KUSAFIRI NA WAUME, NILIDHANI…
TUTAWAULIZA BINAMUZE KAMA WAMEMUONA!
NIMEONGEA NA MAMA WENGINE KULE MBELE NA HAKUNA ALIYEMUONA KULE JUU.
KWA HIYO LAZIMA YUKO HAPA NA VIJANA WAKUBWA.
LABDA HIVYO AU ALIBAKIA--
"--YERUSALEMU!"
NINGEKUULIZA MWANZO.
MARIA, HAPANA.
YESU HAJAWAHI KUFANYA JAMBO KAMA HILI. UNGEJUAJE?


WALIANZA KUTAFUTA YERUSALEMU.
MARIA NA YOSEFU! NINI KINACHOWAREJESHA HAPA?
HAMUKUWA NJIANI KURUDI NAZARETI?
MLISAHAU KITU?
HAPANA.. .EEH, NDIO...
NI YESU. HAYUKO KWENYE MSAFARA.
AAH.
HAYUKO HAPA. POLENI.
ASANTE.
NAONA KAMA AMBAYE TULIMPITA NJIANI.
JE KAMA AMEUMIA NJIANI NA TWAMTAFUTA MJINI?
MARIA USIWAZE HIVYO. ENDELEA KUANGALIA.
NA KUOMBA.
SAMAHANI, YAWEZEKANA KUWA UMEMUONA KIJANA WANGU?
ANA MIAKA KUMI NA MIWILI NA ANGEKUA ANATEMBEA PEKE YAKE. ANA KIMO CHA WASTANI, NYWELE NYEUSI.
DADA ULIVYOELEZA NI NUSU YA WATOTO HAPA MJINI!
TULIFIKIRIA KAMA UMEKUWA MAHALI PAMOJA SIKU NZIMA WAWEZA KUWA UMEMUONA!
NAKUONEA HURUMA--NINA WATOTO NANE--LAKINI KWELI SIWEZI KUKUSAIDIA!
HAINA HAJA! MJI NI MKUBWA MNO!
TUMEANGALIA MAHALI KOTE ANGELIKWENDA!
NGOJA, SIO KOTE!

LUKA 2:45-46


--UMELETA WAZO ZURI KIJANA, WAZO SIKUWA NIMELIWAZA MIMI MWENYEWE MPAKA HIVI KARIBUNI!
LAKINI HUWEZI KUKANA UMUHIMU WA SHERIA!
USISAHAU, TULIPEWA SHERIA NA BWANA WETU NA SIO BURE!
LAKINI SIO SHERIA TU LAZIMA TUFUATE.
SIDHANI SWALA MUHIMU NI "TUTAFUATAJE SHERIA?"
BADALA YAKE TUJIHUSISHE NA "TUTAMFUATAJE ALIYETUPA SHERIA?"
HA! KIJANA UMENENA!
KWELI UMENENA!
YESU!


LUKA 2:46-47



KIJANA, UMETUFANYA HIVI KWA NINI?
NIMEATHIRIKA NA WASIWASI!
TUMEKUTAFUTA KILA MAHALI!
NILIDHANI UMEUMIA... AU ZAIDI!
SINGEWEZANA NA WAZO LA KUKUPOTEZA!
ENHE? MJIBU MAMAKO.
UTAJITETEA AJE KUPOTEA NAMNA HIYO NA KUMFANYA MAMA YAKO NA MIMI KUKUTAFUTA KOTE MJINI?
MBONA MLIKUWA MWANITAFUTA?
HAMKUJUA NINGEKUWA HAPA? KWA NYUMBA YA BABANGU?


LUKA 2:48-50


NJOO MWANANGU.
NI WAKATI WETU KWENDA NYUMBANI.
ASANTE KIJANA KWA KUONGEA NASI!
UMETUANGAZIA MENGI! AKILI YANGU HAIJACHANGAMSHWA HIVI KWA MDA MREFU!
LAKINI KULINGANA NA SHERIA ALIYOPEWA MUSA, "WATII MAMA YAKO NA BABA YAKO"!
HUYU KIJANA NI WA AJABU!
AH NAJUA!
INAONEKANA ANAELEWA MAMBO AMBAYO MIMI NA WENZANGU HATUYAFAHAMU!
ATAKUWA NA HATIMA YA AJABU!
HUNA HABARI!



LUKA 2:47-48


NA YESU ALIKUA.
ALIKUA KIHEKIMA.
ALIKUA KWA KIMO.
LUKA 2:52


AKAKUA NA FADHILA YA MUNGU.
NA FADHILA NA WANAADAM.
NA MARIA ALIVITHAMINI HIVI VYOTE MOYONI.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."








SUPERBIBLE.TV